
# MIPAKA YOTE YA DUNIA

## Zab 97, 1,2-3ab, 3cd-4,5-6
## Noêl

**Mtunzi: Capax Kizis**




1. Mwimbieni Bwana wimbo m**pya**;
kwani amefanya maaja**bu**.
Amepata ushindi kwa mkono wake wa kuu**me**,
kwa mkono wake mtaka**tifu.**

2.Bwana amejulisha wokovu wa**ke**;
mbele ya macho ya mataifa amefunua haki ya**ke**.
Amekumbuka wema na uaminifu wa**ke**
kwa nyumba ya Isra**eli.**

3.Mipakayote ya dunia imeo**na**
wokovu wa Mungu we**tu**.
Mshangilie Bwana, nchi zo**te**,
furahini, shangilieni na kumwi**mbia**.

4. Mwimbieni Bwana kwa kinu**bi**,
kwa kinubi na sauti ya vinan**da**,
kwa tarumbeta na mvumo wa baragu**mu**:
shangilieni mbele ya Bwana **Mfal**me.